Gazeti la kwanza la Islam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

JUZU 82 No. 235 | DH.HIJ-MUHAR.1444AH | DISEMBA 2022 | ZAHOOR 1401 HS | BEI TSH. 700/=

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Enyi mlioamini, si halali kwenu kuwarithi wanawake kwa nguvu; wala msiwazuie (kuolewa) ili mpate kuwanyang'anya baadhi ya vile mlivyowapa, isipokuwa wawe wamefanya uovu ulio wazi; na kaeni nao kwa wema ; na kama mkiwachukia, basi huenda mchukie kitu na AllahAmetia heri nyingi ndani yake. (An-Nisaa 4:20)

Amir na Mbashiri Mkuu Tanzania Akutana na Waziri wa mambo ya ndani.

Na
Shabani Athumani Shunda
Mubaligh Silsilah-Tanzania

Waswahili husema usione vyaelea ujue vimeundwa. hakuna chochote ambacho huja kwa ghafla. Wala hakuna tokeo lolote ila nyuma yake kuna juhudi za mtu au watu wengi. Kanuni hii ndio inayoongoza ulimwengu wa kimwili, kiroho na hata kifikra. Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya Tanzania imekuwa ikifanya hatua kubwa za kimaendeleo katika Nyanja za utendaji wake, katika Tabligh na Tarbiyyat na uwanja mpana wa kuimalisha mahusiano na viongozi wa serekali ili kuitambulisha Jamaat katika uwanda mpana zaidi na kuimalisha uhusiano na pia sababu kuu ya kufanya hayo yote ni sawa na kauli ya Amiri na Mbashiri Mkuu Maulana Tahir Mahmood Chaudhry ni kwamba hatuna lolote la kuficha kwao.



Ujumbe uliokutana na Waziri kulia kwenda kushoto Naib Amir na Mkuu wa chuo cha jamia Sh. Abid Mahmood Bhatti, Waziri wa mambo ya ndani Mh. Hamad Masauni, Amiri na Mbashiri Mkuu Mkuu Sh. Tahir Mahmood Chaudhry, Naib Amir Sh. Abdul-Rahmani Muhammad Ame, Sh. wa Mkoa wa Dodoma Sh. Muzaffar Khawaja Na mwl. dodoma mjini Mwl. Hamisi Bungu sahib.

Itakumbukwa ya kuwa miezi michache iliyopita akiongoza ujumbe wa Jamaat Maulana Sh. Tahir Mahmood Chaudhry walitembelea Bunge La Tanzania, walitambulishwa ilipopatikana fursa ya kukutana na Waziri Simbachawene Ambaye kwa moyo mkunjufu alipokea ambako walikaribishwa na mwaliko wa kuhuzuria Jalsa Salana ya 51, Ahadi ambayo alitekeleza alifika kwenye Jalsa na Kuhutubia.

Katika muelendelezo wa ukarasa mpya ulifunguliwa katika kuimalisha mahusiano na viongozi wa serekali, mnamo 04/11/2022 siku ya Ijumaa uongozi wa Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya Tanzania ukiongozwa na Amiri na Mbashiri Mkuu Tanzania Maulana Tahir Mahmood Choudhry Sahib pamoja na manaibu wake Sheikh Abdur Rahmaan Muhammed Amme Sahib na Sheikh Abid Mahmud Bhatt Sahib walielekea Dodoma kutokea Morogoro, ambapo kulikuwa kuna hafla za michezo

Endelea Uk wa 5..

TAMASHA LA MICHEZO LAFANA

Na
Mwandishi wetu

Kila mwaka wanachuo (masheikh, walimu na Wanafunzi wa chuo chetu cha Jamia Ahmadiyya Tanzania, hufanya tamasha la michezo mbalimbali wanapoelekea mwishoni mwa muhula wa Pili.

Mwaka huu 2022 Tamasha hilo lilifanywa kakatika, siku za Jumatano na alhamisi tarehe 2-3November. Mgeni rasmi katikaTamasha hilo alikuwa ni Maulana Sheik Tahir Mahmood Chaudhry Sahib Amir na mbashiri Mkuu nchini . Hafla ya ufunguzi ilifanyika siku ya JumatanoTarehe 2 NOV. 2022 na kama ilivyo Kawaida na taratibu Za Jamaat, hafla ilianza saa 2:00 asubuhi kwa Usomaji wa QuraniTukufu iliyosomwa na ustaadh Yakini Rajabu Sandari na Kufuatiwa na hotuba fupi iliyotolewa na maulana Sheikh Azizi A. Shahzad Sahib.











Katika hotuba yake Sheikh Sahib aliwataka wanafunzi waonyeshe ustadi na umahiri katika michezo lakini kamwe wasisahau kuzingatia mafundisho ya Qurani tukufu, ya mtume mtukufu Saw na Hadhrat Masihul-manud as juu ya huruma na Mapenzi baina yao, Shabaha ya Mashindano haya ni Kujenga, Kuimarisha na Kuboresha afya zao na utimamu wa mwili Kwa ujumla na vivinginevyo.

Baada ya hotuba hiyo fupi ya sheikh Sahib, yalifuata maombi ya kimya yaliyoongozwa na Mgeni rasmi (Amir ma mbashiri mkuu hapa nchini .Michezo mbalimbali ilishindaniwa kama vile mpira wa wavu, kurukachini (Long Jump), Kurukajuu (high Jump), Kichurachura, Kulenga shabaha kwa manati, nguvu za mikono, Mirudabba, baari (senta), riadha mita 100 na 1600, Kuvuta Kamba,

Endelea Uk wa 7..

Hutuba ya Jalsa Salana 2022 **uk. 3...**

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

Mungu Ibariki Tanzania

Ukoloni ni mfumo wa nchi moja kuivamia nchi nyingine kwa maslahi mapana ya kiuchumi. Kamwe ukoloni haumfikilii aliyetawaliwa. Ukisikia wamejenga barabara basi elewa dhamira ni kutorosha mali za wakulima na wafanyakazi. Ukisikia wamejenga shule basi jua nia ni wakudumaze zaidi na hatimae uwe zezeta. Usifikiri ni ukarimu ikifunguliwa Hospitali. La hasha wao wanataka upate nguvu ili ukalime Mkonge na Kahawa. Ukoloni daima ni mfumo wa mabavu na uonevu. Ni Mfumo ambao unaishi kwa upanga na unaweza kuondolewa kwa upanga. Historia imethibisha usahihi wa fikra hii.

Kilele cha Ukoloni ardhi unakuwa huna tena. Majina yako hayafai unapewa majina mapya . Huwezi kujitegemea kama kupe unyonye mahali pengine. Utamaduni wako unadharauliwa. Hisitoria yake ni giza na utu wako unawekwa rehani.

Hivyo kudai uhuru na kuupata kama tulivyofanikiwa Tarehe 09/12/1961 ilikuwa ni kurejesha utu wetu, heshima yetu na kuthamini vilivyovyetu. Wakati tunasherekea ukombozi wetu tujiulize ni kwa kiasi gani tumeyafikia malengo ya kupata Uhuru? Je tunaweza kusimama mbele ya mataifa mengine na kusema sisi ni watu huru? Tunajitegemea na tunashirikiana na watu wengine tukiwa sawa? Je tunaenzi utamaduni wetu? Chukulia mfano wa lugha ya Kiswahili. Sijui ni kubeza au kudharau kuchanganya maneno ya Kiswahili na Kiingereza. Kuna watu hawaamini kuwa mawesoma mpaka wapachike pachike maneno mawili matatu ya Kiingereza. Nia ni mbwembwe na kuwakoga wengine. Tunawapa taswira gani Watoto wetu?. Unahaki gani ya kuwakilisha watu ambao unazungumza hawaelewi? Mbunge anasimama bungeni kumtetea mtu wa Katoro, Mchotike, Lusaunga halafu anadondosha maneno ya Kiingereza. Huyu anayechanganya Kiingereza na Kiswahili anania ya kufikisha ujumbe? Bila kujali wewe ni nani mwendo huu ni kosa na aibu. Kazi ya lugha ni kufikisha ujumbe sasa ujumbe haufiki faida yake iko wapi? Tanzania inahesabiwa kuwa mlezi wa Kiswahili na mwana umleavyo ndivyo akuavyo. Dunia sasa inafurika kuja Tanzania kujifunza Kiswahili. Tuikuze lugha hii. Kuna kipindi ilirahisisha ukombozi wetu. Fursa sasa inajitokeza kwa lugha hii kuharakisha Umoja na Muungano wa Afrika. Hakuna kitu chenye thamani ambacho Afrika inaweza kujivunia kuliko lugha ya Kiswahili. Hisitoria imetutwisha mzigo wa kupanda mbegu, kumwagilia maji , kupalilia na hadi ikuwe na itutolee Matunda. Matunda haya yatakuwa kiburudisho kwa wana wote wa Bara la Afrika. Na Uhuru wa Afrika utakamilika tukiwa na lugha moja ya Kiswahili. Wakati tunasherekea uhuru wetu, tulielewa ya kwamba tunawajibu mkubwa wa kukamilisha uhuru wa Afrika.

Ni dhahili Tanzania haiwezi kuwa kisiwa. Ni lazima tufanye biashara na kushirikiana na watu wengine. Lakini tunapofanya hivyo dawamu tutangulize maslahi mapana ya taifa letu. Tufaidike na biashara tunazofanya na wengine. Mikataba tunayofanya inasaidia au inadidimiza taifa? Hayo ndiyo mambo yanayotakiwa kuzingatiwa na taifa lililojipatia uhuru ili liamue mambo kwa maslahi yake. Waliopewa majukumu hayo ya kusaini mikataba wana dhima kubwa kwa mustakabali wa taifa letu. Watangulize uzalendo na daima wakumbuke maneno ya Mtukufu Mtume[saw] “Kuipenda nchi ni sehemu ya Imani.” Mungu ibariki Tanzania.



QUR'AN TUKUFU

كُنتُمْ خَيْرَ أُمَّةٍ أُخْرِجَتْ لِلنَّاسِ تَأْمُرُونَ بِالْمَعْرُوفِ وَتَنْهَوْنَ عَنِ الْمُنكَرِ وَتُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ ۗ وَلَوْ آمَنَ أَهْلُ الْكِتَابِ لَكَانَ خَيْرًا لَّهُم ۚ مِّنْهُمُ الْمُؤْمِنُونَ وَأَكْثَرُهُمُ الْفَاسِقُونَ

(Aal-Imran:110)

Nyinyi ni umati bora mliotolewa kwa ajili ya watu, mnaamuru yaliyo mema na mnakataza maovu, na mnamuamini Mwenyezi Mungu. Na kama Watu wa Kitabu wangaliamini ingali kuwa bora kwao. Kati yao wako waaminio, na wengi wao ni

NUKUU YA HADITHI

عَنْ أَبِي بُرْدَةَ عَنْ أَبِي مُوسَى قَالَ كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ إِذَا بَعَثَ أَحَدًا مِنْ أَصْحَابِهِ فِي بَعْضِ أَمْرِهِ قَالَ بَشِّرُوا وَلَا تُنَفِّرُوا وَيَسِّرُوا وَلَا تُعَسِّرُوا

(SAHIH MUSLIM, KITABUL JIHAD, HADITH NO.4525)

Imesimuliwa na hazrat Burda kutoka kwa Abu Musa aliyesema kwamba: Mtume saw alipokuwa anamtuma ye yote kati ya Maswhaba kwa ajili ya baadhi ya shughuli alikuwa akisema; Bashirieni Habari njema wala msiwachukize na kuwarahisisheni wala msiwape dhiki.

عن ابى سعيد الخدرى قال :سَمِعْتُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَقُولُ مَنْ رَأَى مِنْكُمْ مُنْكَرًا فَلْيُغَيِّرْهُ بِيَدِهِ فَإِنْ لَمْ يَسْتَطِعْ فَبِلِسَانِهِ فَإِنْ لَمْ يَسْتَطِعْ فَبِقَلْبِهِ وَذَلِكَ أَضْعَفُ الْإِيمَانِ

(SAHIH MUSLIM, KITABUL IMAN, HADITH NO.177)

ImesimuliwanahazratAbuSaeedKhudrir.a.aliyesema,nilimsikiamtumesawakisema; anayeshuhudia ubaya kati yenu basi auondoe kwa mkono wake na asipoweza basi kwa ulimi wake na asiyeweza basi auchukie moyoni mwake na hali hii ndio udhaifu wa Imani.

MAHUBIRI; IBADA KUU MIDA HIZI

NI juu ya kila muislamu kutumia muda wake kwa ajili ya kuondoa matatizo inayoikumba Islam siku hizi. Kwa kweli hii ndio ibada kuu

HOJA YA KUMBWA KWA ISSA

Mwandishi akiendelea ana sema Isa ndani ya Qurani Kaumbwa kama alivyo umbwa Adam 3:60 Bila shaka hali ya Issa kwa Mwenyezi Mungu ni kama hali ya Adam aliumbwa kwa udongo kisha akamwambia kuwa basi akawa .Akifafa nua alivyo elewa muandishi wa Bibli ni jibu anasema Hivyo kwa mujibu wa ayah ii Issa aliumbwa kama alivyo umbwa Adam yani kwa udongo na kama Adam alivyo tenda dhambi ndivyo na Issa alivyo mwisho wa kunukuu.

Kwa hali hiyo inaonesha jinsi gani mwandishi alivyo kua haelewi Qurani na hilo sio ajabu . kwani Mwenyezi Mungu Anasema katika sura 47-17:46;Na unapo soma Qurani tunatia baina yako na baina ya wale wasio aminin Akhers pazia iliyo sitiria . Natumetia vifuniko Mioyoni mwa asiye wafahamu. Na katika masikio yao kuna uzito na unapo mtaja mola wako wa pekee katik Qurani basi wao hugeuza migongo yao kwa chuki huo ndio uhalisi . Kwani aya imeonyesa ni jinsi Issa alivyo patikana kwa kutumia neno la qun faya quni kama vile Adam alivyo kuwa kwa Mwenyezi Mungu alivyo sema kuwa akawa nafsi hai ndivyo na yesu alivyo patikana kisani nay eye aliambiwa kuwa tumboni akawa tumboni mwa mama yake Mariyam Ajabu eti mwandishi haelewi Mariyam . Ajabu eti mwandishi haelewi Nikwamba Mwenyezi Mungu alichokusudia hapo ni kuwepo kwao yani wote wawili kauli moja tu iliyo tumika ya kuwa kisha wakawa Yaani Adam hakuwa na wazazi yani hakuwa na baba wala mama hivyo uwepo wake ulitokana na neno la kuwa akawa katika mavumbi pia Issa hakuwa na baba na baba ndio huweka Mimba kwa mwanamke . Hivyo kwakuwa Mariam huku mjue mtu kwa mwanamkwe . Hivyo kwakuwa Mariam haku mjua mtu Mume Na yeye Mimba ilipatikana kwa neno la kuwa ikawa mimba huo ndio mfanano wa Issa na Adam na si vinginevyo

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Dr. Swaleh Kitabu Pazi
Kompyuta: Ahmad Abdul Nasibu.
Mchapishaji: Sheikh Raghib Zia ul Haq
Msambazaji: Mwl. Omari Ali Mnungu
Wajumbe:
1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga
2. Mahmood Hamsin Mubiru.
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu36@gmail.com

MTUME MUHAMMAD SAW MFANO WAKE WA IMANI THABITI KWA ALLAH KATIKA NYAKATI ZA SHIDA NA MISUKOSUKO



Na **Sheikh Karimuddin Shams**
Mbeya,
Tanzania

اِنّ الذين قالوا ربنا الله ثم استقاموافلاخوف عليهم ولاهم يحزنون۔ الاحقاف:۴۶

خلائق کے دل تھےیقین سے تہی۔بتوں نے تھی حق کی جگہ گھیرلی
ضلالت تھی دنیا پہ وہ چھاربہی۔کہ توحید ڈھونڈےسے ملتی نہ تھی
ہوا آپ کے دم سے اس کا قیام۔ علیک الصلاۃعلیک السلام

Kila sifa njema inamthibitikia Mola wetu Mlezi, aliyeepuka na kila ubaya na upungufu wa namna yoyote, ambaye kwa fadhila zake zisizohesabika, Ametujaalia na Jalsa hii adhimu tena na kutpatia nafasi za kuwa warithi wa maombi yaliyopokelewa kabisa ya hazrat Masihe Maud A.S. Allah Mtukufu Atuwezeshe kuwa warithi wa maombi yake yote na kujikusanyia baraka na heri nyingi za mkutano huu. Aamin.

Wasikilizaji watukufu! Jinsi mlivyosikia, nimepewa jukumu nzito ya kuelezea: **"MTUME MUHAMMAD SAW MFANO WAKE WA IMANI THABITI KWA ALLAH KATIKA NYAKATI ZA SHIDA NA MISUKOSUKO"**.

Nguzo kubwa na bora Zaidi kati ya nguzo za Imani ni kumuamini Allah kama ilivyobainishwa katika hadithi za mtume mtukfu.Hazrat Umar bin Al-khattab R.A. anastusimulia kwamba: Malaika Jibriel alimuuliza mtume saw kuwa: ماالایمان؟

Imani ni nini? Mtume saw. akajibu:Imani ndio kumuamini Allah, Malaika wake, vitabu yake , mitume wake, siku ya Mwisho, na kadri ya heri na ya shari. (Bukhari na Muslim)

Kuna riwaya nyingine inaeleza kwamba alipoulizwa mtume saw. kuwa: اَیُّ الْعَمَلِ اَفْضَلُ ؟ ,kitendo kipi ni bora? Akajibu: اَلایمَانُ بِا اللهِ وَ رَسُولِہٖ; kumuamini Allah na mtume wake. (Bukhari na Muslim)

Kisha bwana wetu alisema اَلْاِیْمَانُakitufafanulia zaidi kwamba: بِضْعُ وَّ سِتُّونَ شُعْبَۃ

Imani ina sehemu sitini na kitu:اَدْنَاھَا اِمَاطَۃُ الْاَذٰی عَنِ الطَّرِیْقِ sehemu yake ya chini kabisa ni kuondolea mbali kiuziacho njiani. Imani ni neno la kiistilahi la kiislam ambalo linamaanisha kusadikisha na kisheria maana yake ni kukiri na kusadikisha yale yote ambayo ni miongoni mwa mahitajio ya dini.

Pia maana yake ni kupata amani na kutoa amani. Imani inaongezeka kwa kutii na kupungua kwa uasi. Bwana wetu mtume mtukufu saw alisema: الایمانُ یزیدُ و ینقصُ Yaani Imani hua inaongezeka na kupungua pia.

Kwa kifupi:اَلْاِیْمَانُ تَصْدِیْق بِاللسَّانِ وَ مَعْرِفَۃ بِالْقَلْبِ

Hivyo basi sifa kuu na ya msingi kati ya sifa za Imani ni kumuamini sifa zake،Allah, kwa dhati yake zote kwa undani wa moyo bila kukubali upungufu wowote ndani mwake.

Hazrat Ahmad A.S. anasema:

"Yeyote anayependa kuwa awe na afya nzuri na siha kamili, apate kuongezeka kwenye fedha na mali na awe kila kinacho rahisisha Maisha na kuleta raha ya nafsi kwa kila namna kisha asipate jaribio lolote halafu apende kuwa Mungu Amridhiye, yeye ndiye mpumbavu, hawezi kufaulu kamwe. Wale watu ambao Mungu Aliwaridhia kwao, wao walipitishwa katika mitihani ya namna namna na kukabiliwa na shida na taabu za aina mbali mbali."

Tukisoma Maisha matakatifu ya bwana wetu mpendwa tunapata kujua kuwa Maisha yake yote yalikuwa mfano wa imani thabiti kwa Allah hata katika nyakati za shida na misukosuko.Maisha yake yote yalikuwa tafsiri halisi ya kauli hii kwamba:

اشدالناس بلاءً الانبیاء ثم الامثل فالامثل۔مسنداحمد بن حنبل جلد۶

Yaani manabii ndio wanaopata majaribio makali kuliko watu wote kisha wale wanaofanana nao tena wanaofanana nao.

Akieleza hali yake mwenyewe mtume mtukufu alisema:

Jinsi nilivyoogopeshwa mimi katika njia ya Allah, hakuna mwingine aliyehofishwa na jinsi nilivyopata kuudhiwa katika njia ya Allah hakuna mwingine yeyote aliyeudhiwa kwa kiasi kile.(Jamee Tirmizi, Abwabu zuhd)

Mwana historia Maarufu **bwana Gibban** aliandika akitoa ushuhuda wake kwamba:

"Hakuna mtume aliyepata mitihani mizito kabla yake kama alivyopata Muhammad (S.A.W)". (Gibban,bahawala Nuqushe Rasool namba J.11 uk.548)

Bila shaka yoyote bwana wetu mtume Muhammad S.A.W. alijaribiwa Zaidi hata kuliko manabi wote wa Allah na kuudhiwa na kuteswa katika njia yake, yeye alipata kusikia maneno makali dhidi yake pamoja na shida na taabu za kimwili lakini alizikubali hizo zote kwa bashasha kwa ajili ya Mwenyezi Mungu wala hakutamka neno lolote lisilo na maana wala hakupata kushitaki kwa lolote juu ya mitihani hizo zote bali aliendelea kujisogeza mble kwa heshima na utukufu mkubwa mno kwa kumuamini Mwenyezi Mungu. Bwana wetu mtukufu ni kama jabali la heshima na utukufu. Alitukanwa na watu wa duni wa mji wake na kuitwa kuwa majununi, mchawi, kazzab, na alipata kila aina ya matusi naye hakuzivumilia tu bali alikuwa anawaombea dua kuwa: E, Allah uwasamehe watu wangu, kwani hawanifahamu. (Bukhari)

Wenye kumdhihaki walipokuwa wanamuita Muzammam kuliko jina lake tukufu Muhammad saw basi alikuwa anasema: Mwenyezi Mungu ananilinda na shutma zao, na hao wanamtusi ambaye ni muzammam kwani Allah Amenipa jina la Muhammad yaani aliyesifiwa sana. (Bukhari Kitabul Manaqib)

Maisha yake Mtume yanatoa ushuhuda kwamba:

wakati wa ujana wake ambapo vijana wanakuwa na tamaa ya dunia kwa ajili ya mafanikio ya Maisha yao na kufuata sana mambo ya starehe ya Mustaqbali yao, bwana wetu mtume saw alikuwa anachukuwa masrufu wa siku kadhaa na kuingia ndani ya pango la Hiraa na kushinda humo humo akiendelea kumbuabudu Allah S.W.T. wakati huu mtume saw alikuwa ameshamuoa bi Khadija lakini alikuwa anashinda masiku na masiku kwenye pango la Hiraa kutokana na Imani thabiti kwa Allah.

Maadui zake mtume saw walikuwa wanasema: عَشِقَ مُحَمَّد رَبَّہٗ yaani Muhammd akishalevya na mapenzi ya Mola wake.

Ndugu wasikilizaji! Ibada ni jambo la lazima kabisa kwa binadamu anayemwamini Allah. Bila shaka yoyote mtume wetu alitimiza wajibu huu bara'bara toka mwanzo hadi sekunde la mwisho wa Maisha yake.

Kuna matukio chungu nzima yaelezayo hali ya ibada na Imani yake kwa Allah ningependa kuweka mbele yenu mfano mmoja tu kwamba: mtume saw aliugua sana **wakati wa mwisho** wa Maisha yake na alifariki dunia kwa maradhi hiyo, riwaya zinaeleza kwamba, wakati wa ugonjwa huu, mtume saw akaja msikitini kwa ajili ya sala akiwa ameweka mikono yake mabegani mwa maswhaba wawili na miguu yake yalikuwa **yanaburuz** chini. Huu ndio mfano kwa wanaositasita kuenda msikitini.

Wakazi wa Makka walifanya mipango kadhaa ya dhulma, mateso na ya ukatili kabisa dhidi ya mtume saw ikiwemo kufanya njama za kuwapa talaka mabinti zake Mtume waliokuwa wameshaolewa hivyo kwanza walimuanda **Utba bin Abu Lahab** ambaye alimpa talaka binti yake Mtume bi Rukayya.(Ibne Hasham J.2.uk.296)

Ume kalthum alikuwa ameolewa na mtoto wa pili wa Abu Lahab hivyo basi Abu Lahab alimlazimisha kwa ajili ya kutoa talaka na hatimaye Utaiba alimpa Talaka bi Umme Kalthum. Lakini hayo yote hayakuweza kuleta tetemeko lolote katika Maisha ya mtume bali alikabiliana nayo kwa moyo mkubwa na kuzidi katika kumuamini Allah. (Tabakate Kubra Le ibne Saad j.8.uk.37)

Mtume saw alikuwa haruhusiwi kusali kwa uhuru bali alikuwa anaingia kwenye mabonde kwa ajili ya sala ya alasiri na kusali peke yake au kuwa wawili wawili. (Mustadrak hakim j.4.uk.52)

Kuna somo kubwa kwa ajili ya wale wanaoacha kusali na kutokujaali ibada, wanatakiwa kujichunguza kuwa wanavikwazo gani na wanazuiliwa na nani kwa ajili ya kutokutekeleza sala tano kila siku!

Umme Jamil mkewe Abu Lahab,alikuwa anasambaza miiba njiani mwa mtume saw. Na sawa na riwaya nyingine alikuwa anamshutumu mtume saw na kusema kwamba tumeshamkata muzammam na kuchukia dini yake na kumuasi.(ibne hasham na Mustadrak)

Safari moja **Ubaiy bin Khalf** akaja na mifupa yaliyokuwa yameoza kabisa na akazisaga na mikono yake kisha kuzirusha akipuliza upande wa mtume saw na kusema kwa utani mkubwa kwamba, ewe Muhmmad! je, tutahuishwa tena baada ya kufa kwetu kama hizo? Mtume saw akajibu naam, Mwenyezi Mungu Atakufufueni tena na kuwaingizeni motoni. (Ibne Hasham j.1uk.385)

Aas bin Wa'il alikuwa anamuita mtume kuwa mkiwa. Walid bin Mughira alikuwa anasema kama angeshuka Malaika basi angemshukia mtu mkubwa wa mji huu. (Ibne Hasham j.1.uk.384)

Dhulam, fitina, mateso na taabu za namna hizo zote ziliendelea maishani mwa mtume lakini

Endelea Uk wa 4..

Kutoka Uk wa 3..

yeye alikuwa shujaa wa pekee wa Mungu aliyejisogeza mbele na mbele kuliko kukata tamaa na kukaa kimya, vitabu vya sera na historia vinashuhudia kwamba Pamoja na dhulma na vikwazo wa kila namna mtume saw alipiga hatua za juu zaidi katika kumuamini Mwenyezi Mungu na watu wa Makka walipokataa kusikia mahubiri yake ya kumuamini Allah na kutamka لا الہٰ الاالله basi mtume saw alienda mjini Taif lakin watu wake pia walikadhibisha. Riwaya zinaeleza kwamba Rais wao **Abdi yaliil,** aliwakusanya vijana na kuwaambia kwamba wampigie mtume mawe hivyo wale vijana walianza kumrushia mawe njiani yote. Siku hiyo mtume saw alifanyiwa dhulma kubwa mno na damu yake tukufu ilimwagika hadi kufika miguni pake. Kwa hakika hakuna nabii yeyote kati ya mitume wote wa Mungu, aliyedhulumiwa kiasi hiki. Mungu wa Arshi mwenye Jalai pia alikasirika na kumtuma Malaika Jabril kwa Mtume aliyemfikishia ujumbe wa Allah kwamba kama angetaka basi Malaika wa milima wangewaangamiza hao watu wa Taif!

Ndugu wahudhuriaji wa Jalsa! Angalieni Imani kubwa ya mtume kwa Allah kwamba alisema: hao watamuamini Mungu siku moja, hivyo hawatakiwa kuangamizwa اللہمbali aliwaombea dua kuwa: اھدقومی فانہم لایعلمون

Kutokana na dua hiyo watu wa Taif walimuamini Mungu Mmoja na wakawa imara sana kwenye Imani yao hata wakati alipofariki Mtume saw na watu wengi waliritadi dini ila watu wa Taifa hawakuelegea hata kidogo Pamoja na watu wa Makka na Madina.

Sir William Mu're, adui mkubwa wa Islam, alitoa ushuhuda wake juu ya safari hiyo kwamba: inaonekana wazi Zaidi, adhma na ushujaa wa Muhammad kwenye safari yake ya Taa'if. Mtu pekee, aliyefedheheshwa na kukadhibishwa na watu wake, anatoka kutoka mji wake kwa ushujaa katika njia ya Mwenyezi Mungu….na kuingia mjini mwa wale wanaoabudu masanamu kisha anawaita kwenye Mungu mmoja na kuwatolea nasaha za kufanya tauba. (Life of Mohammad uk.117.toleo Jipya 1877)

Ama baada ya kufariki kwa hazrat abu Twalib, silsila ya kumudhi na kumdhehaki mtume saw iliongezeka mno hadi kumshambuliwa kwa mashambulio makali mno.

Siku moja **mdhalimu Fulani** alitupa majivu kichwani pake mtume saw naye alipofika nyumbani, bi Fatuma alishuhudia hali hiyo, basi alianza kusafisha kichwa chake akilia kwa huzuni ila mtume saw alikuwa anamtuliza na kumwambia ewe mwanangu! usilie, Mungu ni mlinzi wa baba yako.(ibne hasham j.2.uk.26)

Safari moja mtume saw alimwambia mkewe bi Aisha kwamba niliishi Makka kati ya **majirani 2** wabaya, ambao ni Abu Lahab na Ukba bin Abi Muiit، waliokuwa wanaleta mavi ya ngombe na kutupa mlangoni mwangu Pamoja na uchafu wa nyumba zao .

Mtume saw alipokuwa anatoka nje ya nyumba yake na kuyashuhudia hayo alikuwa anasema: enyi Watoto wa Abde Munaf! Mnatoa haki ipi ya ujirani? Kisha alikuwa anausafisha ule uchafu.

Siku mtume saw alikuwa amekaa kwenye **mlima wa Safaa** Jirani na Ka'aba. Abu Jahli adui wake mkubwa alipita kwake na akanza kumshutumu na kumtukana mtume saw pasipo sababu yoyote. Mtume saw aliyasikia yote kwa heshima na utukufu wala hakumjibu. Tukio hili lilishuhudiwa na mjakazi wa hazrat Hamza baba yake mdogo wa mtume saw. Hazrat alikuwa mshujaa mkubwa, Wakati wa jioni hazrat Hamza aliporudi nyumbani tokea mawindoni na kwa ushujaa na Fahari akibeba mikuki na misha'ale. Yule mjakazi aliyeshuhudia tukio lile la asubuhi hakuweza kujizuia basi alisema akimtania hazrat Hamza: wewe unaonesha ushujaa gani ilhali Abu jahli amemsemea sana bin amu yako na kumtusi vibaya? Hazrat hamza alimuuliza yote na ingawaje alikuwa baado hajasilimu ila alikuwa na tabia nzuri ya kiasili na kusikia sikia mahubiri pia hivyo alishikiliwa na ghera na jazba yake ya asili na mara moja akatoka nje na kufika Kaaba pale walipokuwa wamekaa marais wa Makka na kumpiga Abujahli kwa mkuki wake tena kwa nguvu kubwa na kusema wewe unamtukana Muhammad kwa sababu hajibu, sasa kama unaweza njoo nijibu mimi shambulio langu kisha alitangaza kwa sauti ya juu kuwa: mimi pia naingia kwenye dini yake Muhammad saw. Hilo lilikuwa tunda taamu ya subra na kutukujibu shutma za maadui.

Bwana Ghandi, kiongozi maarufu wa mabaniani aliandika: mara nyingi uzima wa mtume uliingia hatarini lakini Imani yake kwa Allah ilikuwa imara sana isiyotetemeka wala haikupungua. Yeye alikuwa na bashasha na kutabasamu daima hata kwenye shida nyingi na taabu kubwa mno kwani alikuwa na Yakini kamili kwa msaada wa Allah.

(Bahawala baۏguzida rasul ghairon me Maqbool uk.32)

Kuna matukio kadhaa yameelezwa ndani ya vitabu vya sera na historia kwamba maadui walipanga mara nyingi kwa ajili ya kumuua mtume saw katika enzi za Makka na mjini Madina pia ila Mwenyezi Mungu alikuwa Anamlinda mtume wake na kumwabia:

وَاللهُ يَعْصِمُکَ مِنَ النَّاسِ :Allah atakulinda na watu.

Wakazi wa makka walipofanya juhudi za kila namna za kumsumbua, kumdhulumu na kumtesa mtume saw na kushindwa mbele ya Imani yake kubwa juu ya Allah na hila na njama zao zikaenda bure tu basi walifanya mpango wa kujitenga na kuweka vikwazo vikali dhidi ya wale wote waliokuwa wanamsaidia mtume saw hivyo mtume saw na watu wake wote walilazimika kukaa kwenye **bonde la Abu Twalib** kwa miaka mitatu kama mahabusa na watu kadhaa walifariki kutokana na njaa na shida za zama zile, lakini shida na taabu hizo hazikuweza kutelezesha miguu ya mtume saw bali aliendelea kuishi kwa Imani thabiti kwa Allah.

Mtume saw alilazimika kuagana na ndugu na wapenzi wake na **kuuacha mji wake Makka**, aliyekuwa anaupenda sana mno. Hebu anagalieni! Siku ile ilikuwa gumu na zito kiasi gani alipouacha Makka! Mtume saw alisimama kwenye jiwe kubwa na kusema akiutazama mji wake kwamba: E, Makka u mji wangu mpendwa na makazi yangu mazuri! Kama watu wangu wasingenitoa basi nisingetoka humo kamwe.(Musnad Ahmad J.4.uk.305)

Mtume mtukfu saw alilazimishwa kupigana vita kutokana na dhulma,ufisadi na mchafuko uliokuwa umeenea nchini na kuitetea dini ya Allah na alitujengea mifano madhbuti ya kumuamini Allah katika nyakati hizo za shida na taabu kubwa. Mtume saw ni mtume wa kwanza **alieyanzisha desturi ya ibada** na kuendelea kusali hata kwenye nyakati za shida. Mtume saw mwenyewe alisalisha sala mara kadha katika hali ya kupigana vita na na kutoa mwongozo kwamba kundi moja litasali na jingine litashika silaha na kulilinda jingine: (sura an-nisaa:102) kuna namna sita zimeelezwa za kusali sala ya hofu na ya vita kwenye vitabu vya hadithi. Sasa je kuna yeyote awezaye kuonesha mfano wa namna hii ya kusali vitani na kuthibitisha Imani yake kwa Allah?

Tuchunguzapo hali ya **vita vya Badri** tunapata kujua kwamba watu mia 313 ambao hawana silaha na kutembea kwa miguu wanaenda kupigana na wanajeshi 1000 wenye silaha, waliopanda farasi. Sasa je kuna yeyote awezaye kuwatoa watu wake na kuwapelekea vitani tena kwa hali hiyo dhaifu bila ya kuwa na Imani thabiti kwa Allah?

Hatuwezi kufahamu hata kidogo kwamba vita vya namna hii inapiganwa bila ya Imani imara kwa Allah.

Mtume saw alikuwa anakabiliana na shida na taabu na misukosuko hizo zote kwa ridha ya nafsi yake bila kutetemeka hata kidogo, safari moja **kidole cha mtume** saw kilipojeruhika vitani alisema:

هَل اَنْتِ اِلاّ اِصْبُع دَمِيتِ

- وفی سبیلِ اللهِ ما لقیتِ

Hiki ni kidole tu kilichopata jeraha na kumwagika damu, na kimeyapata hayo katika njia ya Allah tu.

Kuna tukio maarufu la **vita vya Uhad** kwamba wakati Fulani mtume saw alipata jeraha nyingi na kuanguka chini hata masahaba wengine pia walijeruhika sana na hali ikawa tete, maadui walianza kupiga kelele juu ya ushindi wao na walianza kuwataja masahaba kwamba tumewaua hawa, walitaja jina la hazrat Abu Bakri, hazrat Omari na hata la mtume kwamba tumemuua lakini mtume saw alikuwa anawanyamizisha kwamba wasiwajibu kutokana na hofu ya kuwa isije watatushambulia tena lakini walipopiga takbira ya kuwa:- اُعْلُ حُبُل - Yaani mungu wetu Hubul ameshashinda.

Basi mtume saw alisema: kwa nini hamjibu, kwanini hamjibu? masahaba waliuliza tuwajibu vipi? basi alisema kwa jazba na ghera kubwa ya Imani kwamba semeni:

اَللهُ اَعْلیٰ وَ اَجَلْ- اَللهُ اَعْلیٰ وَ اَجَلْ

Allah yuko juu na ndio mwenye Jalali kubwa!

Huu ndio mfano wa nadra kabisa wa kumuamini Allah katika hali ya shida na taabu kubwa mno.

Mhariri wa gazette la khalisa Samachari aliandika mnamo 1915: tuchunguzapo maisha ya mtume basi sifa kubwa Zaidi mno inayoonekana kati ya khulka zake ni Imani kwa Allah na sifa hii imekamilika kabisa katika dhati yake.(Bahawal baguzida rasool uk.24)

Mtume saw alipata msiba wa wapenzi wake kadhaa, alifiwa na mamake, babu yake, baba mdogo, mkewe bi Khadija na wavulana na wasichana wake amabo idadi yao inafika kwenye 11. **Mwanae Ibrahim** aliyezaliwa mwishoni mwa umri wake kutoka kwa mkewe bi Maria Kibtiyya,

Endelea Uk wa 5..

alikuwa mpenzi wake mkubwa na kuhusiana naye alisema akipewa bishara na Mungu kwamba:

لو عاش لكان صديقانبيا۔ kama angeishi angekuwa nabi mkweli. (Ibne Majah, kitabul Janaiz)

Lakini alipofariki mwana huyu adhimu aliinamisha kichwa chake mbele ya ridha yake Mungu na kufanya subra kubwa na kuonyesha Imani thabiti kwa Allah akisema: macho yanatiririsha machozi, moyo unahuzunika, lakini hatutasema lolote ila yale tu yanayomridhisha Mola wetu ila sisi tumehuzunika kwa kuondoka kwako. (Bukhari,kitabul Janaiz).

Hazrat Masihe Maud A.S. aliyetumwa katika zama hizi ili kuhuisha dini na kukimu sheria aliweza kujenga mifano mizuri ya kumuamini Allaha S.W.T. ningependa kueleza tukio moja tu. **Safari moja alipata kuumwa sana kichwa** chake na alipata tiba ya aina nyingi lakini hakupona. Hivyo tabibu mmoja mahiri aliitwa kutoka mji mwingine naye alipofika alisema, msiwe na wasiwasi nitamponyesha haraka basi seyyedna Ahmad A.S. aliposikia maneno yake ya ushirikina kwamba nitaponesha mara moja, alisema mimi sitaki kutibiwa kwake Kamwe. Je, huyu anajielewa kuwa Mungu? Hivyo kiasi kile kilichokuwa kimepangwa kumlipia kuwa ada yake kililipwa na tabibu huyu alirudishwa kisha huzur alisema kuwa: Mungu wetu ndio pekee anayeponyesha.

Safari moja mtume saw alipokuwa anamuabudu Allah basi maadui wakachukua fursa hii ya kumfungia kitamba shingoni mwake na kuvuta hadi macho yake yakawa meukundu, mara hazrat Abu Bakr akaja pale na kumsaidia Mtume saw

اَتَقْتُلُونَ رَجُلا اَن يقولَ ربّی الله akisema: Kwamba je, mnamuua kwa sababu anasema, Mola wangu ni Allah?

Siku nyingine maadui walileta tumbo la ngamia na kuweka juu ya mtume saw akiwa kwenye hali ya sujda naye hakuweza kuinua kichwa hadi wakaja watu na kuliondoa. Allah Mtukufu anasema akitoa ushuhuda wake juu ya shida na taabu za namna hizo kwamba:

اَرَءَيتَ اللذی ینهیٰ عبدا اذا صلّٰی

Je, umemwona yule anayemzuia mja anaposali.

Safari moja mtume saw alipokuwa anapumzika kivulini cha mti akinigniza panga lake juu na alipopata usingizi kidogo mara akaja **mbedui mmoja** aliyeshika panga lake na kuanza kusema: Nani atakulinda nami leo?

Mtume saw akasimama na kusema kwa utulivu kamili: Allah! Mbedui yule aliogopa na sauti yake yenye jalali na panga lilianguka chini kisha mtume saw akalishika na kumuuliza sasa ni nani awezaye kukuulinda nami? Yule bedui alijibu wewe tu. Mtume saw akatabassamu na kumsamehe tu.

Ndugu zangu wasikilizaji! Nilipokuwa naandaa hotuba niliweza kusoma matukio mengi ya Maisha ya mtume saw na nilipata kutetemeka kabisa kwamba, bwana wetu alikuwa anakabiliana na shida, taabu na misukosuko mengi, mara anaitwa Muzammam, mchawi, mwongo n.k. hakuwa na raha hata kwa ajili ya kumuabudu Mola wake, mara anafiwa na wapenzi wake, alifungiwa kwenye pango la Abi Twalib, alilazimishwa kupingana vita kadhaa kana kwamba alikuwa hana raha kidhahiri lakin Pamoja na hayo yote upande mwingine alionesha Imani, Yakini na furaha na raha juu ya ridha yake Mungu na kila wakati alikuwa anamtolea Shukrani nyingi kana kwamba hana shida wala taabu. hili ni somo kubwa sana kwetu sisi kwamba daima dwamu tuwe wenye kumshukuru Mungu na kuridhika kwa kudra yake kila siku.Ningependa kuimalizia kwa nuku ya hazrat Ahmad A.S.yeye anasema: **Hatimaye Tauhiid** (umoja wa Mungu) itashinda. Miungu mingine itaangamia na mwabudiwa wa uwongo watatenganishwa na Uungu wao…. Itakuwepo ardhi mpya na mbingu mpya. Sasa zinakaribia siku ambamo jua la ukweli litachomoka kutoka kwa upande wa Magharibi na Ulaya utapata kujua juu ya Mungu Mkweli na baada yake mlango wa tauba utafungwa kwani wenye kuingia humo wataingia kwa nguvu kubwa na watabakia wale tu ambao wamefungiwa **milango kwa tabia nao wanalipenda** giza si nuru. Hivi karibuni mila zote zitaangamia isipokuwa Islam na hila zote zitaharibika ila hila ya kimbingu ya Islam ambayo haitapinda wala kukatika, hadi kuuvunja udajjali. Wakati unakaribia ambamo umoja wa kweli wa Mungu utaenea kwenye kila nchi ambayo wanauhisi mioyoni mwao wakazi wa jangwani na wale walioghafilika na mafundisho yote. Siku hiyo haitabakia(haitakuwepo) kafara ya bandia wala mungu yoyote

مجموعہ اشتہارات جلد wa bandia.”(**۳۰۵).۳۰۴.۲**

سنو اب وقتِ توحیدِاتم ہے۔ ستم اب مائلِ مُلکِ عدم ہے

خدا نے روک ظلمت کی اٹھادی۔فسبحان اللذی اخزی الاعادی

Mwenyezi Mungu Atuwezeshe kuiga mifano ya bwana wetu na kuzihuisha katika dhati yetu Aamin

Kutoka uk. 01

na mambo mengine ya kijaamat katika Jamia Ahmadiyya Tanzania. Lengo la safari hii ilikuwa ni kukutana na Waziri wa Mambo ya ndani Mhe. Hamad Masauni. Itakumbukwa vizuri kuwa Mhe. Masauni sio mgeni katika masuala ya utambulisho wa Jumuiya na shughuli zake za kiroho na kijamii kwani si mara ya kwanza ujumbe wa Jumuiya kumfikia na alishawahi kushiriki Jalsa salana ya mwaka 2016 iliyofanyika katika viwanja vya Kitonga Jijini Dar-Es-Salaam akiwa Naibu Waziri wa Mambo ya ndani.

Kikao kilipangwa kufanyika Magufuli city huko Mtumba Jijini Dodoma, na katika siku hiyo hiyo kulikuwa na kikao cha mawaziri wote pamoja na Waziri Mkuu. Kutokana na Kikao kilichokuwa kinaongozwa na Waziri Mkuu, Waziri Masauni alikutana na ujumbe wa Ahmadiyya wa mara baada ya Sala ya Magharibi. Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya iliwasili Mtumba mji wa kiserekali katika ofisi ya Wizara ya mambo ya ndani katika nyakati za nje ya muda wa ofisi, Ujumbe huo uliojumuisha watu watano, waliongozeka walikuwa Sheikh Khawaja Muzaffar Sahib Mbashiri wa Mkoa Dodoma na Mwalimu Hamisi Bundu Sahib ambaye ni Mwalimu wa tawi la Dodoma Mjini. Ujumbe wa Jumuiya ulifika katika sehemu ya kusubiria na punde tu walipata ujumbe wa kuelekea katika ofisi ya Waziri husika ambapo uliingia na kuonana naye, Mhe. Masauni alipewa salamu za Jumuiya ya waislamu Ahmadiya pamoja na kubadilishana mawazo katika masuala kadhaa, Mhe. Waziri alionyesha ushirikiano wa hali ya juu sio tu kwa maneno yake aliyoyatamka kwamba ‘yupo tayari kutoa ushirikiano kwa jambo lolote ambalo litahitaji msaada kutoka katika wizara yake’ bali kwa kuonyesha uungwana wa kukubali kukutana na Ujumbe wa Jumuiya katika saa za nje ya muda wa kazi. Ni namna bora ya kuthibitisha kauli yake kwa vitendo, na kupitia hilo tunaweza kujua ni jinsi gani viongozi wetu wa kisiasa na kitaifa hutoa vipaumbele katika kuzisikiliza na kutatua changamoto zozote za Jumuiya za kidini.



Mh. Wazir Masauni akipokea zawadi ya tafsiri ya Kurani Tukufu kwa Kiswahili kutoka kwa Amiri na Mbashiri Mkuu Sh. Tahir Mahmood Chaudhry Sahib.

Kwa sababu Kikao kilianza kwa kuchelewa basi pia ujumbe wa Jumuiya ulizingatia hali ya siku yenyewe ya Mhe. Waziri kwani alishinda katika kikao kizito na kirefu na pia kesho yake alikuwa asafiri tena hivyo waliamua kufanya kikao kuwa kifupi na wakaagana na kuanza safari ya kurudi Morogoro siku hiyo hiyo. Kikubwa cha kuvutia na kujifunza ni kwamba ofisi yote na wafanya kazi wake wote kila sehemu walikuwepo mpaka muda huo wa karibu na I’shaa (Takribani Saa2 Usiku) lakini walionekana wanajituma na tabasamu zao usoni wakitekeleza majukumu yao. Inajulikana kwamba wao kama watumishi wa serekali wakiongeza mda wa kazi basi kuna kiasi cha posho hupewa, lakini kwa namna walivyokuwa wakionyesha ushirikiano na uchangamfu katika kazi zao basi tunaweza kulibeba hilo. kama Jambo la Hekima. Na hekima ni mali ya mwaminio iliyopotea. Popote unapoikuta ichukue. Nasi tunalo la kuchukua katika tukio hili.

Tunamshuku Allah kwa safari hizi za kuonana na viongozi wa Serikali kwani ni Kutimiza maagizo ya Khalifatul Masih[atba] Ambaye anatuhimiza tushiriki kikamilifu katika maendeleo ya Jamii.

Bustani ya Washairi

NIKUMBUSHE_

Nikumbushe wangu Mola, Uliniumba upeke
Nitumikie Mhula, So lazima nizeeke
Wasidizi m'badala , Wastahili tu shukuri

Nikumbushe si kipawa, Ujuzi wala mahiri
Nisijitunue mbawa, Nikajizinga kiburi
Wale waso nielewa, Wanipendao ni wako

Nikumbushe ya utii, Ufaulu halisia
Jefule haukomboi , Bali nyemi huzuia
Mkufunzi hakosei, Uelewa hupishana

Mwepesi kuomba radhi, Tena nisiwe shupavu
Kamwe nisijipe hadhi, Kujitutumua mbavu
Upole nipe hifadhi , Ubaya siweke nia

Nikumbushe na upweke, Mi niwe furaha yangu
Kweli kwako nijiweke, Wewe uwe ngao yangu
Hasa nafsi nishike , Dunia isihamie

Nikumbushe niridhike, vyote Maliki ni Wewe
Kila mpango niridhike, Nipewe niinyimiwe
Nipe hima niyavuke, Ningali hai ni wako

Nikumbushe dhana njema, M'baya Mimi pekee
Kila mtu ni mwema, Imani nijiwekee
Maadamu tunahema, Anatupenda Karima

Nikumbushe uvivu, Ganzi kausha damu
Nishi nikiwa angavu, Mtendaji wa kudumu
Mwenye imara mbavu, Nisimame mnyoofu

Nikumbushe kazi, Ndio utambulisho
Tena ndio kikombozi, havisaidii vitisho
Fitna, pingamizi, Hazivushi popote

Nikumbushe njema nia, Uwepo wangu ndo Mimi
Niseme najisikia, Mfanyaji na situmi
Chukizo kufurahia , Itoke kwangu chembeni

Shunda Mshundia Wana
Daluni-Tanga

KUA UYAONE.

1. Nina anza na Rabana, yu pekee duniani
   Kwa jinale Subuhana, wanamuita manani
   Ninawaasa vijana, siniulize kwanini
   Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.
2. Wazazi lihangaika, wakavipata vya kwao
   Wewe pia hangaika, na upate kama wao
   Usiwe unaropoka, mali si zako za kwao
   Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.
3. Usiwe unaropoka, ukatafute vya kwako
   Hapo nyumbani ondoka, usije pata anguko
   Kibaya zaidi Kaka, huwapendi ndugu zako
   Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.
4. Huwapendi ndugu zako, unawapiga makonzi
   Zile mali si za kwako, unawatia majonzi
   Eti zako peke yako, kiherehere kama nzi
   Kudeng'a denge'ni baho, kumwande kuna uvyele.
5. Mara Baba ana hiki, mara mama ana kile
   Wageni hauwataki, singizia hiki kile
   Moyo umetahamaki, kutwa kucha makelele
   Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.
6. Kila saa baba yako, mara kanunua gari
   Kiumbe una vituko, jiandae na hatari
   Sijefika kokoriko, kapatwa na tahayari
   Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.
7. Kalindima alinena, vile vitu ni vya kwake
   Na akarudia tena, ndio msimamo wake
   Natakiwa kupambana, mpaka kieleweke
   Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.
8. Mwisho wa Moto Majivu, kuna siku utajuta
   We endeleza uvivu, kisa tu umevikuta
   Usijetoka mkavu, kusubiri kwenye tuta
   Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.
9. Wasema wazazi wafe, upate kurithi Mali
   Kwanini wewe usife, tena ukafie mbali
   Umekaa kama tufe, pia mekosa akili
   Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.
10. Hausaidii kazi, upo upo tu kiumbe
    Hutaki kufanya kazi, mlaini kama embe
    Huwaheshimu wazazi, unawapiga vijembe
    Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.
11. Jishughulishe kijana, utumike kama Jembe
    Nenda hata karakana, pale kwa Mzee Lumbembe
    Tuletee danadana, uje uone kimbembe
    Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.
12. Dhikrillah ndio dawa, kumkumbuka Manani.
    Kazi sala kama kawa, usijifanye muhuni
    Lazima tuende sawa, kwa miongozo kundini
    Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.
13. Ukianza kufa wewe, wazazi watabakia
    Wadogo zako wenyewe, watapata kutulia
    Ulikuwa kama mwewe, kila kitu narukia
    Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.
14. Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.
    Usijivike majoho, uache kimbelembele
    Huna utulivu Roho, hufai kuwekwa mbele
    Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.
15. Nashindwa kueleweshwa, nainakuwakuwaje?
    Sala unapoamshwa, unasema kwani je?
    Dawa ni kufurumushwa, utajua taishije
    Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.
16. Kama kazi saidii, we unafaida gani?
    Na unafanya bidii, ya kuishi hapo ndani
    Wajitia uko hai, hubadiliki kwa nini?
    Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.
17. Na vyombo hauvioshi, pindi vinapochafuka
    Haupiki kisa Moshi, ubosi umetukuka
    Na unajifanya Nyoshi, muziki usiku kucha
    Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.
18. Ubosi umetukuka, unaishi kwa wazazi
    Bado una ukibaka, kitambo huachi wizi
    Ujibadilishe kaka, uza hata tangawizi
    Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.
19. Baba ana Mali nyingi!, mjeuri mtaani
    Vijembe navyo kwa wingi, wakejeli majirani
    Eti utajiri mwingi, watamba barabarani
    Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.
20. Wewe jiachie tuu, kuna siku utanyoka
    Kiburi si Mali kitu, ni bora ukaongoka
    Hamtabaki na kitu, Manani akivitaka
    Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.
21. Koo linakukauka, kazi ya kujisifia
    Jiangalie we Kaka, na muda unafifia
    Mali zitaja ondoka, takuwa umefulia
    Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.
22. Sisi sote ni ndugu, lazima kukumbushana
    Hata ukane undugu, tumeungwa na Safina
    Tabia hiyo bandugu, nami nasema hapana
    Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.
23. Unajifanya wa moto, wala haushauriki
    Wali moto mboga moto, mwendo mkiki mkiki
    Ndugu taungua Moto!, kiburi kukimiliki
    Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.
24. Hao wazee wakifa, shughuli imeshaisha
    Waweza pata kifafa, Mali kizitaifisha
    Nduguzo kina Hanifa, wataishi bila presha
    Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.
25. Naweza pata kifafa, Mali kizitaifisha
    Unavyopenda misifa, kwa watu kujionesha
    Tayari wameshakufa, umebaki na bashasha
    Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.
26. Umebaki na bashasha, maana litaka Mali
    Wazazi wameegesha, wewe unawaza Mali
    Kweli umeniangusha, ulivyokosa akili
    Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.
27. Ngoja ukue uone, simaanishi ghorofa
    Ujitume upambane, uje uzizibe nyufa
    Fanya litekelemwene, uje upate maafa
    Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.
28. Unajifanya mbabe, wenzako kuwakung'uta
    Unatamba kwa utabe, Nguzo imara ukuta
    Kama kweli ni mbabe, kapigane na Ukuta
    Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.

29. Na una tabia mbaya, hata wazazi hawana
    Na wala huoni haya, wazee kujibizana
    Watu wanaimba kwaya, kukumbushwa unanuna
    Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.
30. Ujana Maji ya Moto, kupoa hauchelewi
    Usijione mtoto, kwa kufanya yasostawi
    Takutana na msoto, pakuanza huelewi
    Kudeng'a deng'eni baho, kumwande kuna uvyele.

Wasalaam,
Abdallah S. Kalindima (K-Mtoto)
kalindimasenior@gmail.com

FUMBO FUMBUENI

Nasema pole mpendwa, Mola akupe shifaa
Hofu maumivu kutendwa,Vyazua kizaa zaa
Tuyaonayo mageni, Fumbo siriye ni nini

Dua kwa wano tutoka, Waacha pengo huzuni
Twaacha kwenye vichaka, Wachanga mola twauni
Tuyaonayo mageni, Fumbo siriye ni nini

Wanatungo wenye tenzi, Medani tokolezeni
Kwa utashi na mapenzi, Fumbo hili fumbueni
Tuonayo ni mageni, Fumbo siriye Ni nini

SHUNDA MSHUNDIA WANA
DALUNI TANGA
+255656557721
Email: shunda267@gmail.com

TUNGEJUA

Tungejua udhairu, tulonao binadamu
Tungetembea kwa hofu, tukimuomba karimu
Atuepushe uchafu, ambao kwetu ni sumu
Ili tukirudi kwake, tuwe weupe ja pamba

Mahmood Hamsin Mubiru(Wamamba)
Uswahilini-Bukoba 18/11/2022.

Kutoka uk. 1

mpira wa meza, mpira wa miguu, mbio Za Víunzi nk.
Jumla ya timu tatu zilishiriki katika michezo hiyo, Timu hizo ni Amanat, Shafqat na Shaja'at Mshindi wa jumla ni timuya Shafqat ambao Kwa mwaka wa pili mfululizo wamefanikiwa Kuwabwaga wenzao wote na kuthibitisha kuwa hawana mpinzan iwa kweli kwa sasa.
Tamasha hilo lilihitimishwa siku ya al-hamisi tarehe 3 Nov. 2022 kwa hafla ya ugawaji iliyofanyika mara baada ya sala za magharibi na Isha kusaliwa Kwa Pamoja. Kama Kawaida mgeni rasmi katika hafla hiyo alikuwa ni Maulana, Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry Sahib-Amir na mbashiri Mkuu nchini Tanzania.
Hafla ilianza kwa usomaji wa QuraniTukufu iliyosomwa na ustaadh Hussein omari Mpenda na kisha mgeni rasmi kugawa zawadi kwa Washindi.



Baada ya zoezi la ugawaji wa zawadi, Amir Sahib alitoa nasaha fupi kwa wanachuo, na katika nasaha zake, kwanza aliwapongeza washindi kwa bidii na maarifa Waliofanya hadi kuibuka washindi na kuwataka Wale wasiopata chochote wasikate tama bali Wajiandae vizuri kwa mashindano yajayo. Alisema kuwa michezo sio tu inajenga afya bali inauweka mwili katika hali ya utimamu na ndio maana wale walio vizuri katika michezo hata utendaji wao pia unakuwa Mzuri sana. Hivyo aliwahimiza wasiopenda michezo wachague angalau mchezo mmoja au miwili na wajikite Katika michezo hiyo, ili kuimarisha afya na Kujenga Utimamu wa mwili kwa faida yao wenyewe. pia Amir Sahib alimpongeza mkuu wa chuo na naib Amir Maulana Sheikh Abid Mahmood Bhatti Sahib Pamoja na Timu (Staff) yake kwa ufanisi mzuri wanaoupata Katika kila Nyanja.
Baada ya nasaha za Amir Sahib, alikaribisha Mwenyeji wa hafla hiyo - Yaani Mkuu wa CHuo sahib wa Chuo cha Jamia Ahmadiyya ili kuzungumza chochote. Naye katika maelezo yake. Alimshukuru sana mgeni rasmi - Maulana Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry Sahib Amir na mbashiri mkuu Tanzania kwa kutenga Muda wake Maalum ili kuja kushiriki katika Tamasha hili muhimu kwa mujibuwa Kalenda ya chuo cha Jamia.



Alisema, "Tunakosa maneno halisi ya kukutolea shukrani, kwa jinsi ambavyo unatuongoza na kutuunga mkono katika takriban mambo yote muhimu na ya msingi, nasi Tupo Tayari muda wote kupokea na kuti maagizo yako yote. Hatuna cha kukulipa, bali Tunakuombea kwa Allaah akujaalie afya njema na akufanyie urahisi katika utendaji. Wa Majukumu yako" Alimaliza Naib Amir Baada ya Maneno hayo ya Shukrani, Amir Sahib aliongoza maombi ya Kimya na Kufunga Kikao. Hafla hiyo ilihitimishwa kwa chakula cha Pamoja kwa washiriki wote na wageni waalikwa Pia.

WALE VIPOFU WATATU NA TEMBO

Zamani kulikuwa na wazee watatu wenye urafiki sana kwamba, pamoja na kuwa na pamoja akili na maarifa yao yote, wote walikuwa vipofu.



Wakati siku moja walikutana karibu na mto na wakizungumza juu ya maarifa yao, ghafla, walisikia kishindo. Mmoja wa wazee watatu alipaza sauti, akiuliza 'Nani yuko?'

Kwa bahati nzuri kwao, yule aliyekuja hakuwa zaidi ya msafiri aliyeongozana na kipenzi chao, tembo mwenye amani lakini mkubwa.



"Samahani ikiwa nimekuogopa." - alisema msafiri. "Tembo wangu na mimi tumekwenda mtoni kunywa."

Wale watu watatu wenye busara, waliposikia kwamba walikuwa karibu na tembo, hawakuweza kudhibiti hisia zao kubwa, mmoja wao akiuliza 'Tembo? Je! Nilisikia vizuri? '

Msafiri aligundua kuwa wote watatu walikuwa vipofu na kwamba, kwa hivyo, hawangeweza kumtambua mnyama huyo licha ya ukubwa wake mkubwa.

"Tulikuwa tumesikia juu yao, lakini hatujawahi kupata nafasi ya kuwa na tembo karibu sana nasi." Alisema mzee mwingine. "Je! Tunaweza kuigusa?"

Kuona udadisi wa wazee hao watatu, msafiri huyo alikubali kuwa wanambembeleza mnyama wake.



Wazee watatu waliinuka na kumgusa yule mnyama.

"Tembo ni kama safu kubwa!" Alisema mzee wa kwanza huku akipapasa mguu wa mara nne.

'Unasemaje, rafiki yangu? Tembo ni kama shabiki, anayekuburudisha na upepo dhaifu! "Alisema yule wa pili, akihisi masikio.

"Wote mmekosea." Alisema wa tatu, akipiga honi yake. "Tembo ni kama eel, au nyoka, mrefu na mnene."

Wakati wazee hao watatu wakijadili walichokuwa wakicheza, mmiliki wa mnyama huyo alibaki akishangaa jinsi ilivyokuwa ya kushangaza kuwa watu watatu walikuwa wakigusa tembo mmoja na kufikia hitimisho tofauti.

<u>Maadili</u>: **watu hutoa maoni yao kulingana na kile tunachojua na uzoefu** Kwa hivyo, tunaweza kufikia hitimisho tofauti. Unapaswa kujaribu kuwa na mtazamo kamili zaidi wa vitu. Ukweli kamili haupo.

Jinsi ya kupika Tambi za Mayai

Na **Mtandao**

MAHITAJI.

Tambi ½ paketi.

Vitunguu maji 2 vikubwa.

Karoti 1.

Hoho 1.

Vitunguu swaumu (kata vipande vidogo) kijiko 1 cha chakula.

Carry powder kijiko 1 cha chai. (sio lazima)

Njegere zilizochemshwa ½ kikombe. (sio lazima)

Mafuta kwa kiasi upendacho.

Mayai 2.

Chumvi kwa ladha upendayo.

JINSI YA KUANZA MAPISHI

1.Chemsha maji ya moto yanayotokota, ongeza chumvi na mafuta kidogo, weka tambi kwenye maji hayo chemsha adi ziive. Chuja maji yote ili kupata tambi kavu.





2.Katika bakuli piga mayai kisha weka pembeni.

3.Katika kikaango,weka mafuta,vitunguu maji ,vitunguu swaumu,hoho, karoti na carry powder,kaanga kwa pamoja katika moto mdogo kwa muda mfupi kwani mboga hazitakiwi kuiva.

4.Ongeza tambi na njegere katika kikaango,geuza kila mara ili kuchanganya .

5.Ongeza mayai kwenye tambi kisha geuza kwa haraka bila kupumzika adi mayai yaive na tambi ziwe kavu.Tayari kwa kula.ukitaka tambi zako zisivurugwe yaani ziwe kama kwenye picha , ukiongeza mayai usizigeuze hadi unapoona yai limeiva kwa chini unageuza upande wa pili kama upikavyo chipsi yai.enjoy!



NINI HATMA YA ASIYE SALI KWA MUJIBU WA ISLAM

Sala ni nini? Sala ni ile dua inayo ombwa kwa kumtukuza Mwenyezi Mungu na kumuhimidia , na kueleza utakatifu wa kumuomba ghafira na kumsalia Mtume saw kwa unyenye kevu . Faida za mtu anaye Sali kwanza kabisa sala nikinga ya dhambi ,katika Quran Tukufu sura 29:46 inasema ''Soma ulivyo funuliwa na usimamishe sala bila shaka sala huzuia mambo ya aibu na maovu ,na kwa yakini kumbuko la Mwenyezi Mungu nijambo kubwa kabisa .Na Mwenyezi Mungu anajuwa mnayo yatenda''.moja ya faida nyingine ya mtu anaye Sali tena imelezwa katika Hadithi na Hadharat Abu Huraira ra anasimulia '' Nilimsikia Mtume[saw] akisema ''je mwafahamu kwamba kama mlangoni kwa mtu Fulani kunapita mfereji wa maji naye aoge humo mara tano kwa siku je utabaki uchafu wowote mwilini mwake ?Masahaba wa kajibu '' ewe Mtume wa Allah hakuna uchafu wowote utabaki .Mtume akasema '' Huu ndio mfano wasala tano Mwenyezi Mungu Husamehe madhambi kupitia hizo na kuyaondolea mbali madhaifu''

Je? nini hatma ya mtu asiye Sali kwa mujibu wa Islam. Kwa mujibu wa Quran tukufu sura 19:60 inasema ''Lakini wakaangamia baada yao wazao wabaya wakaharibu sala na wakafuata matamanio mabaya, kwa hiyo hivi karibuni watakuta maangamizo „

Hatma nyingine kwa mtu asiye Sali kwa mujibu wa Islam katika Quran tukufu sura 74:43-44inasema ''Ni kipi kilicho wapelekeni motoni ? Watasema hatukuwa miongoni mwa walio Sali „Haya ndiyo majibu ya watu watakao tiwa motoni ,ya kwamba hawakuwa wanao Sali .

Quran tukufu inaendelea kusisitiza hatma nyingine ya asiye Sali katika sura 107:5-6 inasema ''Basi ole kwa wanao Sali . Ambao wana puuza sala zao„

Hadharat Aqdas Masihi Mauudi as anasema '' Sala ni faradhi kwa kila mwislamu.Imo ndani ya Hadithi tukufu kwamba watu Fulani walisilimu mkononi mwa Mtume saw na wakasema ''Ewe Mtume wa Allah , sisi tusamehewe kusali kwa sababu sisi ni wafanya biashara , kutoka na wanyama n.k tunakuwa hatuna uhakika wa usafi wanguo zetu wala hatuna wakati''Yeye Mtume saw akawajibu . ''Tazameni kama hakuna sala kutabaki nini tena ? Dini isiyo na sala si dini.

Hadharat Aqdas anaendelea kusema '' Enyi watu wote mnaojihesabu kuwemo ndani ya jumuiya yangu mtahesabiwa mbinguni kuwemo ndani ya jumuiya yangu mtakapo kanyaga kwa ukweli kabisa njia za ucha Mungu . Hivyo , Salini sala zenu tano kwa hofu na kwa welekevu kiasi hiki kana kwamba mnamuona Mwenyezi Mungu , sawa sharti latatu la Baiati ni kwamba utatekeleza sala tano kwa nyakati zake sawa na Amri ya Mungu na Mtume wake saw.

Kwa mujibu wa Hadithi za Mtume saw ni kwa mba mtu hambaye asimamishi sala hapati nafasi ya kuongea na Mola wake .napia mtuambaye hasimamishi sala kwa mujibu wa Islam humpelekea kuwa karibu nadhambi au kufanya matendo mahovu kwa sababu ana ofu ya Mwenyezi mungu . Tumuombe Mwenyezi Mungu tuwe wenye kusali sala zetu za faradhi na nafali ili tukubaliwe na kupata ukaribu na Allah .Amina.

MIONGOZO MUHIMU KWA WABASHIRI NCHINI

Na Sheikh Mussa ibn Issa Mtwara

Nakumbukuka maneno ya Amir na Mbashiri Mkuu Tanzania kuwa kama wabashiri tunatakiwa tuwe wabunifu katika utendaji wetu, na pia ni muhimu kuipa Jumuiya muda wa kuiwaza ili tuweze kupata mawazo mapya kila siku ya kuitumikia, hivi karibuni tulipata kutangaziwa manaibu Amir wawili ambao wangemsaidia Amir na Mbashiri mkuu katika majukumu yake ya kiutumishi. Sheikh Abdur rahman Muhammed Ame alikabidhiwa pawa la malezi na Mahubiri na Sheikh Abid Mahmood Bhatt alikabidhiwa bawa na kutengeneza mahusiano mema kati ya Jumuiya na Jamii inayotunzunguka pamoja na kusimamia miradi ya Jumuiya Tanzania.

Tokea ubunifu huu ulipotendekea mambo yalianza kupata rangi na sura ya kuvutia, ziara na mikutano yenye tija imeendelea kutokea. Nikiangalia miezi kadhaa nyuma, ujumbe wa Jumuiya umeweza kukutana na Waziri Mkuu wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Mh **Kassim Majaliwa Majaliwa**, kiupekee zaidi na kwa ukubwa wa namna yake Ujumbe wa Jumuiya ya waislamu Ahmadiyya Tanzania ulikutana na Makamu wa rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Mh. Dr. Philip Isdor Mpango.**

Kuelekea katika tukio muhimu la kitaifa la Jalsa Salana ya 51 Tanzania 2022 tukio ambalo halikutokea kwa miaka kadhaa kwa sasa janga la Uviko 19, hivyo basi miongoni mwa mawazo na maamuzi yaliyoazimiwa ni kuwaalika Viongozi wa Serekali lakini sio kwa kuwaandikia tu barua kama iliyokuwa ikifanyika bali inabidi kwenda kuwatembelea watuone nyuso zetu zinaongea nini juu ya imani yetu. Ziara ya siku tatu ilipangwa ambapo ilionekana kuwe na jopo la Wabashiri watano ambao watawaikilisha Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya Tanzania, katika azma hii yenye adhama na nia kubwa ya kuitangaza Jumuiya ya Masihi aliyeahidiwa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad (as). Msafara ulifika Jijini Dodoma mnamo Tarehe 19/09/2022, baada ya mapumziko mafupi katika Makao makuu ya Mkoa, safari ilianza kuelekea ukumbi wa Bunge kuonana na **Mh. George Boniface Simbachawene** Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), upande wangu kama mmoja wa wakilishi rohoni nilikuwa na umara wa hali ya juu na nilikuwa nasoma istighfar njia nzima ila kwa nje nilishapigwa na butwaa zito kwa sababu ilikuwa ndio mara ya kwanza kuona ukimbi wa Bunge kwa macho bila chenga na ndio nilikuwa naenda kuingia ndani. Baada ya kupita katika taratibu zote ambazo walinzi walionyesha heshima zote kwa bashasha tulielekea katika ofisi za Mheshimiwa Waziri. Hatukusubirishwa mapokezi lakini wakati tulipoingia tulichangamkiwa sana kinyume cha matarajio yangu, wote tulikuwa kwenye lengo la mwisho la kufikisha ujumbe kwa Mh Waziri. Mara tukaruhusiwa kuingia ndani na Mh. Waziri alikuwa mlangoni kutupokea mwenyewe kwa kutupa mikono kwa

Endelea Uk wa 10..

MATUKIO KATIKA PICHA







Amir na Mbashiri Mkuu Jamaat, Tanzania ***Maulana Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry*** *akiwa na Wabashiri pamoja na Wasaidizi wake katika ziara ya kumtembelea Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania* ***Mh. Tulia Ackson.***

WABASHIRI NA WANACHUO-JAMIA AHMADIYYA WAFANYA ZIARA CHUO KIKUU CHA KILIMO {SUA}.



Amir na Mbashiri Mkuu Jamaat, Tanzania akiwa na Wabashiri pamoja na wanachuo Jamia Ahmadiyya katika ziara katika ziara chuo kikuu cha kilimo (SUA)

Kama ilivyo ada na desturi, kila mwaka baada ya mkutano wa shura, wabashiri wa mikoa mbalimbali nchini huungana na wanachuo na wanafunzi wa chuo cha Jamia Ahmadiyya katika kutekeleza majukumu mbalimbali ikiwemo kufanya ziara katika maeneo muhimu kwa shabaha ya kujionea na kujifunza mambo muhimu ya mazingira, jamii na maisha kwa ujumla.

Mwaka huu wa 2022 ziara hiyo ilifanyika katika moja ya taasisi muhimu sana hapa nchini, nayo ni chuo kikuu cha sayansi ya kilimo-*SUA*. Ziara hiyo ilifanyika mnamo majira ya saa 3 :00 asubuhi hadi saa 10:00 alasiri. Msafara huo uliongozwa na Maulana Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry Sahib-Amir na Mbashiri Mkuu hapa nchini. Wakiwa huko, wabashiri wa mikoa, wakufunzi na wanafunzi wa chuo chetu cha Jamia Ahmadiyya Morogoro walishuhudia mambo mengi muhimu kama vile utunzaji wa mazingira, kilimo cha kisasa cha mazao mbalimbali n.k.

Kwa ujumla ilikuwa ni ziara yenye tija na faida kubwa kwa washiriki kwani walijionea jinsi teknolojia inavyotumika ili kuleta mapinduzi chanya ya kilimo. Ziara hiyo ilihitimishwa kwa kupiga picha mbalimbali za kumbukumbu na chakula cha pamoja.

MIONGOZO MUHIMU KWA WABASHIRI

Kutoka uk. 8

uchangamfu. Baada ya yote alisomewa utambulisho wa Jumuiya na kazi zake katika nchi katika kuutumikia ubinadamu kiroho na kimwili, mara alikumbuka miradi mitatu ya visima vya maji iliyofadhiliwa na Humanity first ambayo alipewa katika jimbo lake la Kibakwe – Mpwampwa alionyesha shukurani sana, alipoanza kutoa maoni yake kuhusu utambulisho wa Jumuiya alisema kuwa "Leo nimefahamu kuwa Jumuiya ya Waislamu Ahmadiya ni Jambo kubwa ambalo linajitegemea, mwanzo nilidhani kuwa ni taasisi ambayo ipo chini ya Bakwata" na aliongea mambo mengi ya kuonyesha furaha na hamasa yake kwa kutembelewa na Viongozi wa dini, aliomba kuombewa dua na kuungwa mkono katika juhudi za kuimarisha amani katika nchi yetu. baada ya hapo Amir na Mbashiri Mkuu alimkabidhi Mh. Waziri Nakala ya Qurani tukufu ya Kiswahili pamoja na vitabu vingine vya Jumuiya.

Tulipokuwa tayari kuondoka baada ya kikao kuisha kwa mafanikio makubwa, Mwandishi wa habari ambaye alikuwa katika chumba cha tukuo aliuliza swali kwamba kwanini mmempatia Mheshimiwa Nakala ya Qurani tukufu huku mkijua fika kuwa yeye ni Mkristo, ilibidi apatiwe jibu ambalo lingemfaa kwa mazingira aliyopo hivyo basi aliambiwa kuwa " Mheshimiwa ni kiongozi wa Umma hivyo inalazimika pia ajue vizuri imani za anao waongoza ndio maana amepatiwa Qurani tukufu" alionyesha kuridhika na mpaka sasa ni rafiki mzuri wa Jumuiya kwani tuliendelea kushirikiana naye.

Msafara ulirudi Makao makuu ya mkoa kwa shukurani kubwa kwa Mwenyezi Mungu kwa kukifanya kikao cha siku hio kwenda vizuri na kirafiki na heshima kubwa kwani Mh. Simbachaweni japokuwa kulikuwa na wageni wengine katika foleni ya kumuona yeye lakini alimsindikiza Amir na Mbashiri Mkuu huku wakibadilishana mawazo mpaka sehemu ya ngazi za kuelekea mlango mkuu wa kutoa, kwa bashasha alitusabahi na kurudi zake ofisini - Alhamdulillah

Usiku wa tarehe 19 kuamkia 20/09/2022 jopo lililala na habari njema, kwani habari za kuhakikiwa kwa uwepo wa mkutano na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazigira) **Mh Seleman Said Jafo** ilishatufikia naye kwa sababu ya kuijua na kuithamini Jumuiya alipanga kuonana na Ujumbe wa Jumuiya kabla hajahudhuria Vikao vya Bunge, Ikumbukwe Mheshimiwa Jafo alishahudhuria Jalsa Salana Tanzania 2018 akimuwakilisha Makamu wa Rais Mheshiwa Samia Suluhu Hassan ambaye ndiye Rais wetu wa sasa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzani, hivyo saa mbili kamili ilipangwa kuwa mda wa kukutana, hali iliyotulazimu tusilale baada ya Alfajiri kwa ajili ya maandalizi ya kuelekea **Magufuli City** katika mji mpya wa Serekali uliopo **Mtumba** umbali wa wastani wa Kilometa 20. Hivyo ujumbe wa watu sita akiongezeka Mwalimu Hamisi Bundu Mbashiri wa Dodoma mjini ulifika **Magufuli city** mapema.

Tulikaribishwa kwa bashasha na heshima zote na kukaribishwa moja kwa moja katika chumba cha kusubiri, tulipewa taarifa yupo njiani kwani alipitia sehemu Fulani kwa ajili ya dharura Fulani lakini hatochukua muda, mara katika muda tuliotajiwa anafungua mlango kijana wa Makamo mwenye koti la suti la kijani mwenye mwili imara wa wastani mwenye haiba yenye kujitambulisha, aliamkia kwa Assalaam alaikum warahmatullah wa Barakatuh, Mheshimiwa Jafo alitupa mikono na samahani kwa kutusubirisha, alitangulia ofisini kwa kutangulizana nasi.

Kikao kilianza kwa kupewa utambulisho wa Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya na imani zake na kazi zake zote za kiimani na kimwili hapa nchini, ambapo alikiri kuwa hakuwahipo kusikia mgogoro wowote kati ya Jumuiya yenyewe wala ingikwazana na taasisi nyingine, alitoa nafasi kwa kila mjumbe kusema chochote, ambapo Amir na Mbashiri Mkuu Tanzania alichukua fursa hio kuipongeza serekali kwa kuendelea kutoa uhuru wa kuabudu huku ikiendelea kusimamia sera yake ya serekali haina dini lakini watu wana dini ambayo inaonyesha kuwa ndio chanzo cha amani na uhuru wa kuabudu, alimuambia We are enjoy peace in Tanzania (Tunafurahia amani hapa Tanzania).

Mh. Seleman Said Jafo alichukua hatamu kwa kuongelea mambo kadhaa, lakini kubwa alisisitiza juu ya sisi kama viongozi wa dini kuendelea 'kuwaombea viongozi kwani kiasili inaonekana baada ya kupewa madaraka tu huwa yanawageuza kuwa vibofu na viziwi na huwa wanafanya mambo mengi bila kujali wala kuangalia faida na hasara zake'. Pia alisisitiza kuendelea kutoa elimu hasa juu ya masuala sintofahamu kama Jihadi kwani bila elimu hakuna watu huleta tafrani katika kila Nyanja.

Alieleza kumbukumbu zake kuhusu eneo la kitonga na kusifu mpangilio wa eneo na hasa maandalizi ya Jalsa salana aliyoyashuhudia. Na pia alizungumzia kuhusu upandaji wa miti na akaomba kama inawezekana katika mkutano ujao wa Jalsa salana basi kupandwe miti kadhaa kumuunda mkono katika kapeni za kimazingira za Tanzania ya kijani.

Amir na Mbashiri Mkuu Tanzania alisimama na kumkabidhi zawadi ya Qurani tukufu na vitabu vingine vya Jumuiya. Mh. Jafo aliomba kuombewa sana hivyo wazo la kufanya maombi ya kimya kimya lilikuja hivyo Amir na Mbashiri Mkuu alituongoza katika maombi sawa tamaduni ya Jumuiya. Mh. Jafo alionyesha unyenyekevu wa hali ya juu kwani tulipoomba picha naye aliruhusu tupige naye ofisini na nje ya ofisi pia. Alitusindikiza na kupata picha ya pamoja naye nje ya ofisi akiwa na furaha sana na kutusindikiza kwa salamu na maombi mengi na kutukaribisha tena, Ujumbe wa Jumuiya ulirudi na kuendelea na shughuli nyingine za kijamaat katika siku hio - Alhamdulillah

Baada ya ukaguzi mrefu wa kutembelea mali za Jumuiya katika Wilaya ya Dodoma Mjini, tuliporejea Makao makuu tukiwa tunakula chakula huku mazungumzo mepesi mepesi juu ya fadhila na baraka za Allah zikiendelea yakiendelea, nilikumbuka jambo ambalo ilibidi nibaki nyuma nimuulize Naibu Amiri Maulana Abid Mahmood Bhatt sahib juu ya maendeleo yake, nilipomuuliza jambo hili akasema nafuu umenikumbusha ngoja nilifuatilie, tukaingia sebuleni wote tukabalizi kwa uchovu, Amiri na Mbashiri Mkuu alikuwa anaongea na Mtu kwenye simu. Mara alipomaliza mazungumzo alitusomea ujumbe kutoka kwa sekretari wa Amiri na Mbashiri Mkuu Mwalimu Yusufu M. Juma ambao ulikuwa anaeleza kuwa amepokea simu kutoka kwa katibu Mkuu wa Bunge kuwa mualiko wetu umehakikiwa hivyo kesho tumeealikwa kushuhudia Mkutano wa 8 kikao cha saba, mimi kwa sababu ilikuwa ni shauku yangu na ndio niliyokuwa nikimkumbusha Naib Amiri Sahib basi nilipitiwa na kaubaridi kamoyo na siku ikaanza kuwa ndefu.

Mnamo tarehe 21/09/2022 ilikuwa ni siku ya kihistoria kwa Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya Tanzania ilikuwa siku ndefu yenye matukio ya kusisimua imani. Ratiba ilianza mapema kwani saa tatu na nusu asubuhi ilikuwa Ujumbe wa Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya uende kuonana na Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Mhe. Rosemary Senyamule Ikulu Dodoma City centre. Kwa sababu ratiba ya Ujumbe wa Jumuiya ukiongozwa na Amiri na Mbashiri Mkuu Tanzania Maulana Tahir Mahmood Chaudhry ulikuwa na ratiba ngumu basi ilikuwa unaharaka mno, ila tulipofika Mhe. Mkuu wa Mkoa alikuwa ametingwa na vikao kadhaa ambavyo vilitufanya tusubiri kwa dakika takribani arobaini, ilipofika wakati wa kutaka kufanya maamuzi ya kuondoka au kusubiria kidogo basi Allah alifanya jambo la kukutana na Mkuu wa Mkoa kuwa rahisi, Ujumbe ulipata nafasi ya kuingia ndani na kufanya kikao kifupi, kwani Mkuu wa Mkoa huyu alishapata kukutana na Ujumbe wa Jumuiya huko Mkoani Simiyu alipokuwa Mkuu wa Mkoa alipokaribishwa na kupata chakula cha jioni pamoja na viongozi wa Jumuiya na kupewa utambulisho wa Jamat katika hafla hio. Hivyo basi kana kwamba ilikuwa ni kwenda kumsabahi na kuendeleza mahusiano mema nayeye baada ya maongezi machache ambapo aliomba sana kuombewa yeye na Serekali kwa ujumla na Mji wa Dodoma, baada ya hayo alikabidhiwa zawadi za vitabu vya Jumuiya. Kwa uso mchangamfu na tabasamu kubwa alitukaribisha kwa ajili ya picha hasa alimuita mpiga picha wake na akasema tusimame ilipo bendera ya nchi kwani watu wengi huogopa kupiga picha nayo. Mkutano uliisha mda muafaka huku ukitufunza kuwa Mungu ana muda wake wa kutenda jambo na halazimishwi kwani muda tuliotoka ulitutosha kuenda kujiandaa Makao makuu na kuenda kuwahi katika tukio linalofuata.

Ilikuwa ni saa nne na dakika ishirini na tano kukiwa na jua angavu na hali ya hewa tulivu gari ya Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya ilifika katika geti la wageni Maalumu la Jengo la Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwa na Wabashiri watano ambao ni Maulana Tahir Mahmood Chaudhry Amiri na Mbashiri Mkuu Tanzania, Sheikh Abdur Rahmaan Mohammed Ame Naibu Amiir Tabligh & Tarbiyyat, Sheikh Abid Mahmood Bhutt Naibu Amiri Kutengeneza Mahusiano mema na msimamizi wa Miradi ya Jumuiya, Sheikh Khawajah Muzaffar Mbashiri wa Mkoa wa Dodoma na Sheikh Shabani Athumani Shunda. Walinzi baada ya kutupokea walituelekeza kuwa inabidi tukapitie geti la wageni ambalo lipo upande mwingine ambapo haikuwa shida kulifikia. Alhamdulillah tulipofika na kufanyiwa ukaguzi na kuruhusiwa, alikuja muongozaji ambaye alitupeleka katika sehemu ya ukaguzi ya pili ya ambao ni mlango wa bunge wa kuingia wageni, kisha baada ya ukaguzi tukaanza kuelekea ukumbini na askari kanzu

Itaendelea toleo lijalo Inshallah

SIFA MAHSUSI ZA SAYYIDNA ABUBAKAR[ra]

Watu Walio Bora Kabisa – Masahaba wa Badri (r.a). Makhalifa Walioongoka – Hadhrat Abu Bakr (r.a)

Kutoka uk. 12

(as) alieleza kwamba Mitume hutumwa katika ulimwengu huu na ujumbe na kazi hiyo inapokamilika, basi unafika wakati wao wa kuondoka, jambo ambalo Hadhrat Abu Bakr (ra) alilielewa na kulifahamu kutoka kwenye aya hii. Zaidi ya hayo, Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (as) anaeleza, kwa kurejelea Hadith ambamo Mtume Mtukufu (s.a.w) alisema kwamba madirisha yote isipokuwa lile la Hadhrat Abu Bakr (ra) yanapaswa kufungwa ilimaanisha kwamba hazina zilizofichika za Mwenyezi Mungu zinazofananishwa na msikiti daima ziwe wazi na dhahiri kwa Hadhrat Abu Bakr (ra). Hii haikuwa na maana kwamba mlango huu ulifungwa kwa ajili ya wengine, hata hivyo ulikuwa wazi zaidi kwa Hadhrat Abu Bakr (ra), kwani mtazamo wake ulikuwa bora zaidi kuliko mtu mwingine yeyote.

Hadhrat Abu Bakr (ra) Mfasiri Mkuu wa Ndoto Baada Ya Mtume Mtukufu (s.a.w):

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alisema kwamba Hadhrat Abu Bakr (ra) pia alikuwa na umahiri mkubwa katika kufasiri ndoto na alikuwa akifasiri ndoto katika zama za Mtume Mtukufu (s.a.w). Ibni Sinaa anasema kwamba baada ya Mtume Mtukufu (s.a.w), Hadhrat Abu Bakr (ra) alikuwa ndiye mfasiri mkuu wa ndoto. Wakati fulani, mtu mmoja alikwenda kwa Mtume Mtukufu (s.a.w) na akasema kwamba aliona ndoto ambamo ndani yake kulikuwa na wingu ambalo mafuta na asali vilianguka na watu walikuwa wakinufaika navyo. Kisha akaona kamba ikining'inia kutoka mbinguni ambayo Mtume Mtukufu (s.a.w) aliishika katika ndoto na akapanda mbinguni na kisha watu wengine wawili wakapanda kwa njia hiyo hiyo. Mtu wa tatu alishika kamba hiyo lakini ikakatika, kisha ikaunganishwa, kisha naye akapanda kwa kutumia kamba hiyo hiyo. Baada ya kusikia ndoto hii, Hadhrat Abu Bakr (ra) alimwomba Mtume Mtukufu (s.a.w) ruhusa ya kuifasiri, na Mtume Mtukufu (s.a.w) alimruhusu. Hadhrat Abu Bakr (ra) alisema kwamba wingu hilo lilikuwa ni Uislamu na mafuta na asali vilivyoanguka kutoka humo ni Qur'ani Tukufu. Watu wanaonufaika na mambo haya walirejea kwa wale wanaopata elimu ya Qur'ani Tukufu. Kamba ya kwenda mbinguni iliwakilisha ukweli ambao Mtume Mtukufu (s.a.w) alikuja nao na kuushika ulimnyanyua Mtume Mtukufu (s.a.w). Kisha watakuwapo walio thibiti baada yake juu ya haki hiyo hiyo, kisha theluthi yao ambao kwa ajili yao kamba hiyo itavunjika kwanza na kurekebika baadaye. Mtume Mtukufu (s.a.w) alisema kwamba Hadhrat Abu Bakr (ra) alikuwa sahihi katika baadhi ya vipengele na alikosea katika vingine katika tafsiri yake, hata hivyo Mtume Mtukufu (s.a.w) hakuona ni muhimu kufafanua zaidi wakati huo.

Hudhur (atba) alisema kwamba Mtume Mtukufu (s.a.w) aliona ndoto akiwa pamoja na Hadhrat Abu Bakr (ra) kwenye mwinuko na Mtume Mtukufu (s.a.w) alikuwa hatua mbili na nusu mbele ya Hadhrat Abu Bakr (ra). Hadhrat Abu Bakr (ra) aliifasiri ndoto hii kuwa ina maana kwamba Mwenyezi Mungu Atamwita Mtume Mtukufu (s.a.w) kwake na kwamba Hadhrat Abu Bakr (ra) atabaki hai kwa miaka miwili na nusu baada ya hapo, na hivi ndivyo ilivyotokea.

Hudhur (atba) alisema kwamba siku moja Hadhrat A'ishah (ra) aliona katika ndoto kwamba miezi mitatu inaangukia kwenye chumba chake. Baada ya kufariki kwa Mtume Mtukufu (s.a.w) alipozikwa katika nyumba ya Hadhrat A'ishah (ra), Hadhrat Abu Bakr (ra) alimwambia kwamba huu ulikuwa ni mwezi wa kwanza kati ya miezi mitatu aliyoiona na huu ulikuwa bora zaidi.

Mwanaume Mtumzima wa Kwanza Kuukubali Uislamu:

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alisema kwamba kuhusu wa kwanza miongoni mwa watu kuukubali Uislamu, imeandikwa kwamba alikuwa ni Hadhrat Abu Bakr (ra). Mtu wa kwanza kwa ujumla alikuwa Hadhrat Khadijah (ra) ambapo baada ya hapo baadhi ya wanachuoni wanatofautiana kuhusu mtu (mwanamume) wa kwanza kumkubali. Hata hivyo, kama ilivyoelezwa na Hadhrat Mirza Bashir Ahmad (ra) katika kitabu "Maisha na Tabia ya Muhuri wa Mitume (s.a.w)" haitakuwa sahihi kusema kwamba wa kwanza miongoni mwa watu kukubali Uislamu alikuwa ama Hazrat Zaid (ra) au Hazrat Ali (ra); kwa vile wao walikuwa watoto wa nyumba ya Mtume Mtukufu (s.a.w) na walikuwa kama wanawe, hivyo wangemfuata kwa vyovyote vile. Hilo linamwacha Hadhrat Abu Bakr (ra), ambaye bila shaka alikuwa wa kwanza kuukubali Uislamu. Aliheshimiwa miongoni mwa Maquraishi, lakini hakusita hata kidogo aliposikia madai ya Mtume Mtukufu (s.a.w) na akakubali mara moja. Kwa hakika, alijitolea muhanga kwa vyote alivyokuwa navyo kwa ajili ya Mtume Mtukufu (s.a.w).

Hudhur (atba) alisema kwamba wakati huo kulikuwa na watu watano wa mwanzo ambao waliukubali Uislamu kutokana na mahubiri ya Hadhrat Abu Bakr (ra) na wakaendelea kuwa masahaba hodari, ambao ni Hadhrat Uthman bin Affan (ra), Hazrat Abdur Rahman bin Auf (ra), Hazrat Sa'd bin Abi Waqqas (ra), Hazrat Zubair bin al-Awwam (ra) na Hazrat Talhah bin Ubaidillah(ra). Masahaba hawa wote pia walikuwa miongoni mwa masahaba kumi (Asharah Mubasharah) waliopewa bishara ya kuingina Peponi na Mtume Mtukufu (s.a.w).

Mtu Aliyekuwa Tayari Kutoa Kila Dhabihu Kwa Imani Yake:

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alisema kwamba Mtume Mtukufu (s.a.w) alitambua dhabihu kubwa zilizotolewa na Hadhrat Abu Bakr (ra) mwanzoni mwa Uislamu. Dhabihu zilizotolewa hapo mwanzo na Hadhrat Abu Bakr (ra) haziwezi kulinganishwa, ingawa wale waliofuata pia walijitolea sana, kama vile Hadhrat Umar (ra). Wakati fulani, wakati ulipotokea mzozo kati ya Hadhrat Abu Bakr (ra) na Hadhrat Umar (ra), Mtume Mtukufu (s.a.w) alisema kwamba wakati watu hawakuukubali Uislamu, Hadhrat Abu Bakr (ra) aliukubali, na wakati watu walipoupinga Uislamu, Hadhrat Abu Bakr (ra) aliusaidia Uislamu, hivyo basi kwa nini alikuwa anasababishiwa maumivu? Huu ulikuwa ni ushahidi wa dhabihu zake alioutoa Mtume Mtukufu (s.a.w) mwenyewe.

Mkombozi wa Watumwa:

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alisema kwamba Hadhrat Abu Bakr (ra) alijulikana kwa kuwaacha huru watumwa. Kwa hiyo, mwanzoni mwa Uislamu, kulikuwa na watumwa saba ambao Hadhrat Abu Bakr (ra) aliwaachisha huru kwa mali yake mwenyewe kwa ajili ya Uislamu. Hata wapinzani wa Uislamu walitambua ubora wa Hadhrat Abu Bakr (ra). Safari moja, wakati Hadhrat Abu Bakr (ra) alipokuwa anaondoka Makka, chifu mmoja alimwuliza anaenda wapi. Hadhrat Abu Bakr (ra) alimwambia kwamba Makka hapakuwa salama tena kwake. Chifu akajibu kwamba ikiwa mtu mwema kama Hadhrat Abu Bakr (ra) ataondoka, basi mji wa Makka utakuwa umeharibika. Hivyo, Hadhrat Abu Bakr (ra) alibaki pale chini ya ulinzi wake, na alipokuwa akisali na kusoma Qur'ani Tukufu, wapita njia walikuwa wakisimama na kusikiliza na kuathiriwa na usomaji wake uliojaa uchungu wa kuvutia sana. Wakati watu walipolalamika, chifu alimwomba Hadhrat Abu Bakr (ra) asisome kwa sauti kwani iliwakasirisha watu wengine. Hadhrat Abu Bakr (ra) alisema kwamba hataacha kufanya hivyo na kama chifu anataka kuondoa ulinzi wake basi aondoe ulinzi huo.

Naibu wa Mtume Mtukufu (s.a.w) katika Kuongoza Sala:

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alisema kwamba Hadhrat Abu Bakr (ra) alikuwa miongoni mwa wale walioheshimiwa na waliobahatika kuteuliwa na Mtume Mtukufu (s.a.w) nyakati fulani kuongoza sala katika Msikiti wa Mtume. Mtume Mtukufu (s.a.w) pia alikuwa katika sala iliyoongozwa na Hadhrat Abu Bakr (ra); katika riwaya moja imeandikwa kwamba Mtume Mtukufu (s.a.w) alipokuwa mgonjwa, alikaa upande wa kulia wa Hadhrat Abu Bakr (ra) alipokuwa akiongoza Sala na kusali nyuma yake.

Upendo na Utunzaji kwa Familia yake:

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alisema kwamba Hadhrat Abu Bakr (ra) alikuwa mwema sana kwa watoto wake. Ingawa mtoto wake mkubwa aliishi kando, Hadhrat Abu Bakr (ra) alishughulikia gharama za nyumbani kwake. Binti yake Hadhrat Asma (ra) alikuwa akiishi chini ya mazingira magumu na hakuwa na mfanyakazi nyumbani kwake, hivyo ilimbidi afanye kazi nyingi ngumu yeye mwenyewe. Alipopata habari hii, Hadhrat Abu Bakr (ra) alimtuma mfanyakazi nyumbani kwake, jambo ambalo alisema likawa nafuu kubwa kwake.

Hudhur (atba) alisema kwamba ataendelea kueleza matukio haya

The First Muslim Newspaper in Swahili Language since 1936

MapenziyaMungu

DH.HIJ-MUHAR.1444AH | DISEMBA 2022 | ZAHOOR 1401 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu^{saw}

Abu Huraira^{ra} anasimulia kwamba: Nilimsikia Mtume^{saw} akisema: Abu Huraira wallahi mimi naomba msamaha kwa Allah kutubia kwake kwa siku moja zaidi ya mara sabini (**Bukhari**).

SIFA MAHSUSI ZA SAYYIDNA ABUBAKAR^{ra}

Watu Walio Bora Kabisa – Masahaba wa Badri (r.a). Makhalifa Walioongoka – Hadhrat Abu Bakr (r.a)

Baada Ya Kusoma *Tashahhud, Tawwudh* na *Surah Al Fatiha* Hadhrat Mirza Masroor Ahmad Khalifatul Masih wa Tano (atba) alisema kwamba ataendelea kuangazia baadhi ya matukio ya maisha ya Hadhrat Abu Bakr Siddique (ra).

Mtaalamu wa Nasaba:

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alisema kwamba kwa mujibu wa riwaya, Hadhrat Abu Bakr Siddique (ra), alikuwa na ujuzi katika elimu ya historia na nasaba za Waarabu, hasa zile za Maquraishi. Wale ambao baadaye walikuja kuwa wataalamu katika uwanja huu wa elimu walihusisha elimu yao katika fani hiyo na Hadhrat Abu Bakr (ra) kwani alikuwa na ujuzi wa hali ya juu sana ya suala hilo. Alijua chanya na hasi za nasaba, hata hivyo hakuwa anataja vipengele hasi.

Hudhur (atba) alisema kwamba siku moja, Mtume Mtukufu (s.a.w) alimshauri Hadhrat Hassan bin Thabit (ra) kwamba kabla ya kuandika mashairi kuhusu Maquraish, anapaswa kushauriana na Hadhrat Abu Bakr (ra) kuhusu nasaba ya Maquraish. Baada ya kusikia shairi hili, ikawa dhahiri kwa wasikilizaji kwamba limeandikwa kwa kushauriana na Hadhrat Abu Bakr (ra).



Masjid Mubarak: Hadhrat Khalifatul Masih V^{atba} akihutubia Ijumaa ya Tar. 11.11.2022 kwa waaminio wote Duniani.

Hudhur (atba) alisema kwamba imesimuliwa kwamba ingawa Hadhrat Abu Bakr (ra) hakuwa mshairi, kwa hakika alikuwa na shauku katika ushairi. Wanachuoni na wanahistoria wanatofautiana kuhusu jambo hili kama Hadhrat Abu Bakr (ra) aliwahi kuandika shairi yeye mwenyewe au laa. Kuna baadhi wanaodai kwamba kuna mashairi yaliyoandikwa na Hadhrat Abu Bakr (ra) yanayoweza kupatikana nchini Uturuki.

Ujuzi wa Kina Katika Mambo:

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alisema kwamba Hadhrat Abu Bakr (ra) alikuwa ni mwenye maarifa sana. Imesimuliwa kwamba siku moja Mtume Mtukufu (s.a.w) alisema kwamba Mwenyezi Mungu Amempa mja Wake mmoja chaguo kati ya kile kilichomo katika dunia hii na kile kilicho pamoja Naye, na mtu huyo akachagua kile ambacho kilikuwa na Mwenyezi Mungu. Juu ya hili, Hadhrat Abu Bakr (ra) alianza kulia, jambo ambalo liliwachanganya baadhi ya watu kwani ilionekana kwao kwamba Mtume Mtukufu (s.a.w) alikuwa anazungumza kwa kawaida kuhusu mtu mwingine. Baadaye wakatambua kwamba Hadhrat Abu Bakr (ra) alimwelewa mtu huyo kuwa ni Mtume Mtukufu (s.a.w). Mtume Mtukufu (s.a.w) alimwambia Hadhrat Abu Bakr (ra) kuwa asilie kwa kuwa yeye alikuwa mstari wa mbele katika wema na kujitolea kifedha. Alisema kwamba kama angeweza kuwa na Khalil (rafiki wa karibu) basi angekuwa ni Hadhrat Abu Bakr (ra), hata hivyo udugu wa Uislamu ni mkubwa zaidi. Alisema kwamba madirisha yote yanayoelekea msikiti yanapaswa kufungwa isipokuwa lile la Hadhrat Abu Bakr (ra).

Hudhur (atba) alisema kwamba Hadhrat Abu Bakr (ra) pia alikuwa na utambuzi na ufahamu mkubwa wa Qur'ani Tukufu. Kwa mfano, pale iliposhushwa Aya isemayo kwamba: **"Leo nimekukamilishieni Dini yenu na kukutimizieni neema yangu"** (5:4); Hadhrat Abu Bakr (ra) alianza kulia, kwani alihisi kwamba hii ina maana ya kuwa kufariki kwa Mtume Mtukufu (s.a.w) kulikuwa kumewadia.

Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa

Endelea uk11



Kitabu Kijacho

Kifungua Mlango wa Kiutalii Kurani Tukufu

Hapo awali iliandikwa kama utangulizi wa Kiingereza tafsiri na ufafanuzi wa Mtakatifu Qur'an ilichapishwa pamoja na maelezo mwaka wa 1947. Baadaye ilichapishwa tofauti kwa ombi maarufu. inafurahisha Kitabu kinachunguza hitaji la Qur'ani Tukufu na jinsi maandiko mengine yalivyoteseka tafsiri, kuongeza, kufuta, nk; hiyo kisha inaweka unabii uliotolewa na wakati uliopita manabii kuhusu Mtukufu Mtume Muhammad^{saw} (rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake). inaongezewa na bora na mchoro wa maisha ya ectionate wa Mtukufu Mtume(saw).

Nakala hii itapatikana kwa bei ya Sh. 15,000/=

Kwa Makala, Maoni, Ushauri; Tuandikie

mapenziyamungu36@gmail.com